JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
MAARIFA YA JAMII - DARASA LA VII

JINA:____________________________________________________SHULE: ___________

MAELEKEZO KWA MTAHINIWA: MUDA: SAA 1:30

1. Mtihani huu una sehemu A, B, na C zenye jumla ya maswali SABA (7).
2. Soma maelekezo na ujibu maswali YOTE katika kila sehemu.
3. Tumia kalamu ya wino wa BLUU au MWEUSI kujibu maswali.
4. Simu za mkononi pamoja na vitu visivyoruhusiwa HAVITAKIWI

**SEHEMU A (Alama 20)**

1. Kutoka kipengele (i) – (xv) chagua jibu sahihi na uzungushie kwa usafi (Alama 15)
   i) Ni zao gani la biashara linalolimwa mkoani Kigoma? a) Tumbaku b) mawese c) pamba d) mkonge e) karafuu [ ]
   ii) Zifuatazo zilikuwa sababu za upinzani wa Waafrika dhidi ya uvamizi wa wakoloni, ISIPOKUWA: a) Kutetea uhuru wao b) Kupinga ushuru c) Kupinga upotevu ardhi d) Kupinga unyonyaji e) Kupata pesa kutoka kwa wakoloni [ ]
   iii) Moja ya mbinu za kupigana dhidi ya hatari zinazosababishwa na uharibifu wa mazingira ni: a) Kukata miti b) Kuchoma vichaka c) Shughuli za uchimbaji madini d) Kupanda miti e) Kuchoma mkaa [ ]
   iv) Wakati wa siku kuu ya wakulima waziri mkuu alisema "kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa Tanzania". Taarifa hiyo ina maana gani? a) Inatekelezwa na matajiri b) inafanywa kwa kutumia matrekta na jembe c) ni shughuli kuu ya uzalishaji d) inafanywa katika vyanzo vya maji pekee e) Mazao yaliyovunwa yanauzwa nje ya nchi [ ]
   v) Wakulima wengi nchini Tanzania husafirisha mazao yao ya kilimo hadi sokoni kwa ajili ya kuuza kwa njia tofauti za usafiri. Je, wanatumia njia gani za usafiri zaidi? a) reli b) njia za maji c) njia za anga d) reli e) barabara na njia za maji [ ]
   vi) Jumuiya ya Afrika Mashariki ilianzishwa mwaka 1967 kwa mara ya kwanza. Wakuu wa nchi zilizowezesha jumuiya ya pili ya Afrika Mashariki walikuwa: a) Benjamin Mkapa, Milton Obote na Jomo Kenyatta b) Julius Nyerere, Jomo Kenyatta na Yoweri Museveni c) Patrice Lumumba, Julius Nyerere na Milton Obote d) Julius Nyerere, Milton Obote na Jomo Kenyatta e) Benjamin Mkapa, Jomo Kenyatta na Yoweri Museveni [ ]
   vii) Mwezi unapokuwa kati ya jua na dunia ni tukio la kijiografia linaloitwa__ a) Kupatwa kwa jua b) kupatwa kwa mwezi c) kivuli Kizito d) kupatwa kwa mwanga e) kupatwa kwa dunia [ ]
   viii) Bahati alichora ramani ya kijiji chake bila kuonyesha ufunguo. Je, ni athari gani itakabiliwa na mtumiaji wa ramani hiyo? a) Kushindwa kutambua mpaka wa kijiji b) kushindwa kutambua ukubwa halisi wa kijiji c) kutokuwa na uwezo wa kutambua alama na ishara zinazotumika katika ramani hiyo d) maudhui ya ramani hayataeleweka e) mazao ya chakula yanayopatikana kijijini hayataonekana wazi [ ]
   ix) Mtalii mmoja aliwasili Tanzania kupitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa , moja kwa moja akaenda kutembelea Mlima Kilimanjaro. Ni njia gani ya usafiri iliyomwezesha mtalii huyo kufika Tanzania? a) Maji b) Anga d) Reli e) Bomba [ ]
   x) Baadhi ya mazao hutumika kama malighafi katika viwanda. Ni mazao gani hutoa malighafi kwa viwanda vya nguo? a) Tumbaku b) Ngano c) Pamba d) Karafuu e) pareto [ ]
   xi) Ngome ya Yesu katika Afrika Mashariki ilijengwa na Wareno huko__ a) Mombasa, Kenya b) Bagamoyo, Tanganyika c) Lusaka, zambia d) Sofala, Msumbiji e) Pemba, Zanzibar [ ]
   xii) Moja kati ya yafuatayo si tabia ya ujasiriamali; a) Kufanya kazi kwa bidii b) uvivu c) kujaribu d) uaminifu e) Ukweli [ ]
   xiii) Je, Rwanda na Burundi zilijiunga lini na jumuiya ya Afrika mashariki? a) 2007 b) 2009 c) 2002 d) 1967 e) 1995 [ ]
   xiv) Fuvu la mtu wa kale zaidi liligunduliwa na ___________ huko Olduvai Goji mnamo 1959. a) Karl Peters b) Horace Byatt c) Dk. Louis Leakey d) Hakuna jibu e) Chifu Mangungo [ ]
   xv) Chombo kinachotumika kupima kasi ya upepo kinaitwa _____ a) Anemomita b) baromita c) kipima upepo d) reingeji e) thermomita [ ]

2. **Oanisha vipengele vya safu wima A na vile vya safu B ili kupata sentensi zenye maana (Alama 5)**

| SEHEMU “A” | SEHEMU “B” |
| --- | --- |
| i) Fursa za kiuchumi katika maeneo yenye dhahabu, kokoto na chokaa [ ]<br>ii) Fursa za kiuchumi katika maeneo yenye wanyama wengi wa aina tofauti [ ]<br>iii) Fursa za kiuchumi katika maeneo yenye mito, maziwa na Bahari [ ]<br>iv) Fursa za kiuchumi katika maeneo yenye mvua nyingi na udongo wenye rutuba [ ]<br>v) Fursa za kiuchumi katika maeneo yenye barabara nzuri, reli na bahari [ ] | A. Usafirishaji<br>B.Ufugaji<br>C.Uchimbaji madini<br>D. Kilimo<br>E. Utalii<br>F. Uvuvi<br>G.Biashara |

**SEHEMU B (Alama 20)**

3. Jaza nafasi zilizoachwa wazi (alama 6)
   a. Kuna shughuli nyingi za kiuchumi zinazofanywa nchini Tanzania. Shughuli ya kiuchumi inahusisha ufugaji na uzalishaji wa mazao inaitwa ______________________________
   b) Bidhaa za kioevu kama vile mafuta na gesi husafirishwa kwa vifaa maalum kama bomba. Bomba la mafuta la TAZAMA husafirisha mafuta kutoka Tanzania hadi nchi iitwayo ______________________________
   c) Daktari Louis Leakey aligundua fuvu la mtu wa kale huko Olduvai Goji mnamo mwaka 1959, na akalipa jina. Aliliita jina gani?

4. Jaza nafasi zilizoachwa wazi (alama 6)
   a) Safu ya angahewa inayofanana na blanketi ambayo hulinda dunia dhidi ya kuangukiwa na asteroidi na vitu vingine kutoka angani inajulikana kama______________________________
   b) Ni kundi gani la mjasiriamali ambalo mtu ambaye ana wafanyakazi 100 na zaidi na mtaji wa zaidi ya shilingi milioni 800 huwekwa? ______________________________
   c) Mishonari, wafanyabiashara na wachunguzi walikuwa ni watu waliokuja Afrika ya Mashariki kama?
   ______________________________

5. Jaza nafasi zilizoachwa wazi (alama 4)
   a) Athumani alitoka Uganda na kwenda kuzuru Afrika Kusini katika maeneo ya pwani ya Bahari ya Hindi. Katika safari hii Athumani anajulikana kama ______________________________
   b) Jua, sayari na satelaiti zote kwa pamoja zinaunda ______________________________
6. Jaza nafasi zilizoachwa wazi (alama 4)
   a) Tanzania ni nchi iliyobarikiwa kuwa na aina nyingi za madini. Ni madini gani yanayotumika kutengeneza nishati ya nyuklia?______________________________
   b) Wanakijiji wa kijiji cha Semeni wamekuwa wakichoma misitu kwa malengo ya kuandaa Ardhi kwa ajili ya shughuli za kilimo. Je, shughuli hiyo inaathari gani?
   ( i)______________________________
   (ii) ______________________________

7. Chunguza picha ifuatayo kwa makini kisha jibu maswali yafuatyo



   a. Taja shughuli ya kiuchumi inayofanyika kwenye picha hii? ______________________________

b) Je, ni jina gani la mahali hapa ambapo shughuli ya kiuchumi iliyoonyeshwa hapo juu inafanyika?
_______________

c) Je, kuna umuhimu gani wa shughuli iliyoonyeshwa hapo juu kwa nchi yetu?
________________________________

d) Andika hasara moja ya shughuli iliyoonyeshwa hapo juu kwa mazingira yetu.
_______________________________

e) Andika kifaa/chombo chochote kilichotumika katika shughuli iliyo hapo juu
_________________________________